East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

East African Journal of Swahili Studies
eajss.eanso.org
Volume 6, Issue 1, 2023
Print ISSN: 2707-3467 | Online ISSN: 2707-3475
Title DOI: https://doi.org/10.37284/2707-3475

EAST AFRICAN NATURE & SCIENCE ORGANIZATION

*Original Article*

# Sifa Za Wahusika Za Kisimulizi Katika Ngano Za Wachuka

*Rebecah Wanja Kirimi[1*], Martin Mugambi Allan[1] na Onesmus Gitonga Ntiba[1]*

[1] Chuo Kikuu cha Chuka, S. L. P. 138-60400 Chuka, Kenya.
[*] Barua pepe ya mawasiliano: rebecahkirimi@gmail.com

**DOI ya Nakala: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467**

**Tarehe ya Uchapishaji:**

*27 Septemba 2023*

**Istilahi Muhimu**:

*Uhusika,*
*Ujumi,*
*Ngano Za Wachuka.*

## IKISIRI

Makala haya yanalenga kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka, kwa kuongozwa na nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma inayotetea upekee wa kiujumi wa kazi za kisanaa. Madhumuni ya Makala yalikuwa kuchanganua sifa za wahusika wa kisimulizi katika ngano za Wachuka na namna wanavyoendeleza ujumi katika ngano husika. Makala haya yalibaini kwamba wahusika katika ngano za wachuka hugawika mara mbili yaani wahusika wawi na wahusika wema ili kujenga ujumi katika ngano. Mbinu elezi ilitumika kuwasilisha na kuchanganua data.

**APA CITATION**

Kirimi, R. W., Allan, M. M & Ntiba, O. G. (2023). Sifa Za Wahusika Za Kisimulizi Katika Ngano Za Wachuka. *East African Journal of Swahili Studies*, *6*(1), 350-361. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467.

**CHICAGO CITATION**

Kirimi, Rebecah Wanja, Martin Mugambi Allan and Onesmus Gitonga Ntiba. 2023. "Sifa Za Wahusika Za Kisimulizi Katika Ngano Za Wachuka". *East African Journal of Swahili Studies* 6 (1), 350-361. https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467.

**HARVARD CITATION**

Kirimi, R. W., Allan, M. M & Ntiba, O. G. (2023) "Sifa Za Wahusika Za Kisimulizi Katika Ngano Za Wachuka", *East African Journal of Swahili Studies*, 6(1), pp. 350-361. doi: 10.37284/jammk.6.1.1467.

**IEEE CITATION**

R. W. Kirimi, M. M. Allan, & O. G. Ntiba "Sifa Za Wahusika Za Kisimulizi Katika Ngano Za Wachuka", *EAJSS*, vol. 6, no. 1, pp. 350-361, Sep. 2023.

**MLA CITATION**

Kirimi, Rebecah Wanja, Martin Mugambi Allan & Onesmus Gitonga Ntiba. "Sifa Za Wahusika Za Kisimulizi Katika Ngano Za Wachuka". *East African Journal of Swahili Studies*, Vol. 6, no. 1, Sep. 2023, pp. 350-361, doi:10.37284/jammk.6.1.1467.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

## UTANGULIZI

Ujumi ni tawi la falsafa linaloshughulika na uzuri, ubaya na ladha. Ujumi ni elimu ya sheria na kanuni za sanaa (Simala, 2006). Dhana ya ujumi ilitoka kwenye nadharia ya hisia za akili katika karne ya 18 na kuitwa "Falsafa ya uzuri" au "Falsafa ya sanaa" au yote mawili kwa pamoja. Uzuri ni ukamilifu wa hisia za akili unaosababisha kulitazama jambo au mambo fulani katika mtazamo chanya kwani mwingine anaweza kulichukulia jambo hilo kimtazamo hasi lakini mtazamo wake hauondoi uzuri wa chanya kwa atazamaye chanya. Uhakiki wa ujumi ni dhana ya kijumla inayotumiwa kueleza mkabala wa kuhakiki kazi ya kifasihi ambao huchunguza kazi hiyo kwa kuangalia uhusiano kati ya sehemu mbalimbali zinazounda kazi hiyo. Aidha vipengele vya ujumi vina uamili mkubwa katika kuwasilisha ujumbe uliodhamiriwa na mtunzi kwa hadhira yake.

Matumizi mazuri ya vipengele vya ujumi huufanya muundo wa kazi ya fasihi kuvutia hadhira lengwa. Kwa upande mwingine, kutomakinika kwa mtunzi katika matumizi ya ujumi huifanya kazi ya kifasihi kutokuwa na umbo zuri. Matokeo yake ni kuwa kazi ya kisanaa hukosa mshikamano na mwingiliano unaotarajiwa. Matini ya aina hiyo huwa haina uwezo wa kuvutia hadhira (Harmon & Holman, 2000; Hegel, 1979). Fasihi simulizi ni zao la jamii. Kulingana na Mathooko (2006), fasihi simulizi huhifadhi na kuendeleza utamaduni wa jamii husika. Fasihi hushughulikia masuala yanayoikumba jamii mojawapo ikiwa ni usawiri wa wahusika kama vile wahusika wa kiume, wahusika wa kike, wahusika wanyama na pia wahusika mazimwi. Kanuni na sheria za sanaa ndizo kitovu cha kubainisha namna zilivyozingatiwa katika ujenzi wa ngano simulizi.

Ngano ni hadithi zinazotoa mifano kadha wa kadha ya maisha ya binadamu na matatizo anayokumbana nayo ulimwenguni pamoja na njia anazotumia kukabiliana na matatizo hayo. Dhamira kuu ya ngano nyingi ni kudhihirisha jinsi binadamu alivyo na uwezo wa kuyamudu matatizo yake pindi atumiapo akili yake vizuri. Kwa njia hii anaboresha maisha yake na kuishi raha mstarehe. Ngano huwa na aina mbalimbali ya wahusika ikiwa ni pamoja na mazimwi, wanyama na binadamu. Inafahamika kwamba kuna aina mbalimbali za ngano kama vile ngano za mazimwi, ngano za usuli, hurafa, hekaya na mighani (Njogu & Chimera, 1999)

## WAHUSIKA WA KISIMULIZI

Wahusika wa kisanaa huwa ni viumbe ambao huumbwa na msanii kwa madhumuni ya kutekeleza majukumu anayokusudia katika sanaa yake (Wamitila, 2002). Matendo, mienendo, lugha, vionjo, uhai na ufu wa wahusika wa kifasihi hudhibitiwa kwa kiasi kikubwa na dhamira ya mwandishi. Lugha wanayopewa huonyesha matumaini na imani ya mwandishi kwa sababu lugha yao huwa ya wengine. Misemo na maelezo ya wahusika wa kifasihi huathiriwa na matamanio ya wengine na hivyo kuzua ukinzani kati ya lugha ya mwandishi na ya wahusika wake (Bakhtin, 1981). Mawazo haya ni ya muhimu kwa makala haya kwa kuwa kila kazi ya fasihi huwa na wahusika wa kipekee. Kwa misingi hiyo mhakiki anashawishika kuwa wahusika katika tanzu za fasihi simulizi huwa na sifa za kipekee za kisimulizi kutokana na upekee wa mandhari na muktadha wa fasihi simulizi. Upekee huu wa sifa za wahusika unakisiwa kuwa na sifa ya kiujumi katika muundo wa ngano simulizi.

Kineene wa Mutiso, (2005) anadai kuwa wahusika wanaotumiwa na watunzi katika utendaji na upitishaji wa ujumbe ni watu, wanyama, ndege, wadudu miti, mashetani, majini na kadhalika. Maelezo yao yanaeleza tu mifano jumla ya wahusika katika kazi za fasihi. Hata hivyo, Madumulla (2011) anaweka mpaka wa wahusika wa kisimulizi kwa kudai kuwa, wahusika katika hadithi Simulizi na baadhi ya Hadithi Fupi kwa kawaida huwa ni wanyama, wadudu, mimea, mashetani na miungu. Tukizingatia mazingira na muktadha wa nyakati za kutungwa kazi nyingi za kimapokeo za fasihi simulizi ni dhahiri kuwa

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

wahusika wa kisimulizi huwa wa aina ile. Hali hii inaweza kuchangiwa na maisha ya vichakani, msituni pamoja na imani za kishirikina zilizotawala tamaduni za jamii nyingi za Kiafrika. Upekee huu wa wahusika unachukuliwa kama kiungo cha ujumi wa ngano simulizi za Kichuka kama ilivyo katika mada ya utafiti huu. Makala haya yaliangazia jinsi msimulizi wa ngano anavyowachora wahusika katika ngano za Kichuka na kueleza jinsi sifa za wahusika zilivyotumika kupamba ngano simulizi za Kichuka kama nyenzo ya mguso na hisia kwa hadhira.

## MISINGI YA NADHARIA

Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya ujumi wa kinudhuma. Kwa mujibu wa Foley (1995), nadharia ya Ujumi wa Kinudhuma ilianzishwa kule Marekani miaka ya 1950-1960 na waasisi wake wakiwaDennis Tedlock na Dell Hymes. Akina Dennis Tedlock na Dell Hymes walibuni nadharia hii kutokana na utafiti wao wa matini simulizi miongoni mwa Wamarekani. Nadharia hii inajihusisha na ujumi katika upangaji wa matini simulizi kishairi kwa misingi ya taaluma za Isimu-Amali, Isimu Jamii, Ethnografia ya Mawasiliano na Uchanganuzi Hakiki wa Usemi ndani ya Muktadha wa Utendaji. Dennis Tedlock alisisitiza zaidi sifa ya usimulizi katika matini pamoja na mpangilio maalum wa mistari. Vilevile, anadai kuwa matini simulizi inapaswa kuwasilishwa kwa mistari kama ilivyotolewa na fanani katika utendaji wa fani ya usemaji. Uwasilishaji huu huzingatia vipengele kama vile, uradidi, shadda, kiimbo na matumizi ya jazanda. Mwisho, anasema kuwa, utafiti wa nyanjani huwa lazima katika uchanganuzi wa fani ya usemaji, lakini sio matini simulizi iliyoandikwa. Matini simulizi isiandikwe tu kwa maneno bali pawe na maelezo ya ziada yanayofafanua matendo-ambatano ili kuonyesha namna ambavyo ilitendwa katika hali halisi.

Baadhi ya mihimili iliyozingatiwa katika Makala hii ni pamoja na:

- Mistari na aya hazipangwi tu kwa mujibu wa sheria za kishairi, lakini pia hutumiwa kuwasilisha ujumi na tajiriba ya pamoja ya jamii husika kwa kutumia takriri, mianzo maalum na jazanda. Mhimili huu ulitumikizwa katika kuchanganua nafasi ya mbinu kama vile takriri katika uendelezaji wa ujumi wakati wa utunzi na uwasilishaji wa ngano za wachuka. Ulitoa mwongozo na mamlaka ya kuhakiki mbinu za kimtindo zenye kutumika katika uwasilishaji wa ujumi pamoja na tajiripa ya pamoja ya jamii ya wachuka.

- Matini simulizi huwa na matumizi maalumu ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio na wa kihistoria. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi. Nguzo hii ilielekeza uchambuzi wa fani inayotumika katika ngano simulzi za Wachuka kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa Wachuka. Aidha, mhimili huu ulielekeza katika kutathmini jinsi mtiririko wa matukio huendeleza ujumi katika ufumaji wa ngano simulizi za Wachuka. Pia, mhimili huu ulitumiwa kubainisha namna sifa za wahusika wa kisimulizi zilitumika kupamba ngano simulizi za Wachuka.

Kwa mujibu wa nadharia ya ujumi wa kinudhuma Matini simulizi huwa na matumizi maalum ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi. Wahusika katika ngano simulizi za Wachuka waligawika katika kategoria mbili kuu kimatendo. Wahusika wawi na wahusika wema.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

## MBINU ZA UTAFITI

Makala haya yalitumia mbinu elezi. Lengo lilikuwa kutambulisha vifungu vya fani katika ngano za Wachuka, kuchunguza, kuchanganua pamoja na kubainisha vipengele vya kimuundo vya ngano vinavyojenga maana, kuleta ujumi na umbo kamili la ngano.

Utafiti awali ulifanywa kwa lengo la kufanyia majaribio vifaa vya utafiti, kuviimarisha pamoja na kujizoesha na mbinu za utafiti zilizotumika katika utafiti kamili. Mhakiki alikusanya ngano tatu kutoka kwa wazungumzaji wa lugha ya Gichuka wanaoishi makazi tofauti. Data ilikusanywa nyanjani kwa njia ya ushuhudiaji. Uteuzi wa kimakusudi ulizingatiwa ili kukukidhi malengo ya uchanganuzi.

## MATOKEO

### Sifa Za Wahusika wa Kisimulizi katika Hadithi ya *Fisi ya Kindi*

Kwa mujibu wa Wamitila (2002) wahusika ni dira msingi katika kazi za kifasihi kwa sababu huwa waendelezaji wakuu wa matukio na matendo yanayokuza na kuendeleza dhamira ama maudhui ya kazi husika. Kadhalika, kama asemavyo Wamitila (2003), wahusika wanyama, mazimwi, majini, wadudu na hata binadamu ni wahusika wa kisimulizi wanaojitokeza katika fasihi simulizi. Katika hadithi ya fisi na kindi wahusika wote ni Wanyama. Kuna muhusika fisi na mwenzake kindi. Katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci wahusika ni mesto wa binadamu na majitu. Hadithi ya wasichana wanne wa ukambani inahusisha wahusika binadamu na wanyama. Katika hadithi ya chura na mbuni wahusika ni wanyama na pia katika hadithi ya fisi na tembo. Kwa mujibu wa Njogu na Chimerah (1999), wahusika huchanganuliwa kwa namna wanavyoingiliana na dhamira. Hili hutokana na maneno, tabia na matendo yao.

Kwa mujibu wa nadharia ya ujumi wa kinudhuma Matini simulizi huwa na matumizi maalum ya fani ambayo hueleweka na wanajamii kwa mujibu wa muktadha wa tukio. Aidha, uchambuzi wa matini simulizi unastahili kufanywa kwa mujibu wa ujumi na utamaduni wa jamii husika, kwa kuchunguza zaidi matendo ambatani kwani yanachangia katika kuipa maana kamili na halisi. Wahusika katika ngano simulizi za Wachuka waligawika katika kategoria mbili kuu kimatendo. Wahusika wawi na wahusika wema.

#### *Wahusika Wawi*

Wahusika wawi wanajitokeza katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Kwenye utangulizi wahusika wote wanaaanza wakiwa wema. Hadithi inapotangulia kwa tukio la wema wahusika wote wanakuwa sawa kimienendo na hulka. Kwa mfano katika hadithi ya fisi na kindi, fisi na kindi wanakuwa na sifa sawa. Wenye upendo: waanza kama marafiki "*Mbiti na kabare ciatumire urata*". Wenye ushirikiano: wanashirikiana kupalilia konde na kupanda mbaazi *"…cierana niciuge itema, ciauga itema. Cierana niibande nthoroko. Ciabanda nthoroko.*"

Sehemu ya pili ya matukio ya hadithi inakuwa msukosuko wa mienendo. Muhusika mmoja anaanza kwenda kinyume na matarajio. Kwa mfano katika hadithi ya fisi na kindi, fisi alichukua nafasi ya muhusika muwi. Mbaazi zilipokomaa fisi alianza kwenda kinyume cha urafiki wao na kindi kwa kuanza ujanja na ulaghai

> *"Thoroko ri ciakurire, Kabare gakathii gagatua nthoroko. Kenukite gagatungana na mbiti. Mbiti ikathi igatua nthoroko wabaria kabare gatuire. Fisi aliacha kuwa mwaminifu na kuwa mwongo "Kabare ntuku ingi kakithii kethiria kethiria nthoroko ciako iri bakubi guthira, kamiuria "mbiti, ai umbiraga utionaga muntu u umbiaga n ni weu tutunganaga nawe ma? Utanona nwari muntu agitua nthororoko ino ciakwa nuntu iri bakubi guthira?" …Aari aari ntamwona. Ntamwona. Ntamwona."*

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

Fisi alikuwa mwenye tamaa, mlafi na mbinafsi. Alikuwa na shamba lake la mbaazi zilizokomaa wakati mmoja na zile za kindi lakini alitamani zile za mwenzake hadi kuwa mwizi "*Wa ntuku, Kabare kathii gagatua, Mbiti ikauma thuba ikathii igatua. Kwa Mbiti gutigutwiwa. Mbiti nitua gwa Kabare."* Fisi alifikia kiwango cha kuwa nafiki. Wakati wa kuruka mto anaendelea kuruka huku akijua kuwa ndiye mwizi. Alipoanguka mtoni mara ya kwanza aliwaomba wenzake kumtoa kwa kuwa alitumbukia baada ya kukosa kujiandaa vyema. Alipoanguka tena alisisitiza kuwa bado hakuwa amejitayarisha ingawa alijua ni kwa sababu ya kuwa mwizi.

> *Mbiti yagamba runcini butu! Yauga, "Ruutana ndutani ii, gantatubite wega*
>
> *Mbiti cietikira ciaruta Mbiti. Aya! yarutwa ri, Kabare kerwa, "ruuga ringi riu nuntu mbiti yauga nika itarugite weega, iruge weega." Kaina;*
>
> *Ntarumaa x2*
>
> *Muthororoko x2*
>
> *wa muru wa mbiti Ginci kiiru ntwaara.*
>
> *Kabare ri, karuga gakinya rugongo ruria.*
>
> *Mbiti yambiria gutantaura;*
>
> *Ntauma x2*
>
> *muthooko x2*
>
> *wa muu wa kabare Giinci kiiru ntwara*
>
> *Yagamba runcini nku! Yerwa riu mbiti i cingi,*
>
> *"Ai nee riu ni weu wiite." Yauga ari rutaana ndutani ii gantatubite weega ri, tingwa ku."*

Hatima ya mhusika muwi ni maangamizi huku ukweli ukibainika na wenye haki kuipata. Fisi alianguka mtoni mara ya tatu kisha wenzake kumwachilia kufa maji ili apate adhabu na wengine wajifunze kuwa na adabu:

> *"Mbiti yagamba runcini ringi nku! Yagwa runcini. Yambiria gukiriria tuguru, "Ndutani rutaani ntantubite wega. Ti niu. Ti niu. Ti niu. Ndutani ntatubite weega."*
>
> *Mbiti ri, yerwa yerwa ni mbiti i cingi atiri, "tutikuruta ni weu wiaga kabare. Mbiti ikinatwarwa ni runci.*

Sifa mbaya za fisi kama mhusika mui zinaichochea hadhira kuchukia kuwa mwovu katika jamii na kupenda kuwa mwandilifu na mwema. Muhusika mui katika hadithi hii anaipamba hadithi kwa kuonyesha nguvu za matambiko ya jamii kama ala kamili ya kupata haki. Fisi anashindwa na nguvu za tambiko la kuruka mto kisha haki na ukweli kupatikana. Hatima ya mhusika mui ni maangamizi. Fisi anatumbukia mtoni na kufa maji huku wenzake wakimkashifu

> *"Alipoanguka majini akaanza kuinua miguu, "Nitoeni tafadhali. Sikuruka vyema." Fisi wengine wakamwambia, "Hatutakutoa. Ni wewe huiba mbaazi za kindi." Fisi akasombwa na maji."*

***Wahusika Wema***

Wahusika wema wanajitokeza kama wahusika bapa. Wanadumisha umbo lile lile la kimienendo kuanzia uatangulizi hadi kwenye sehemu ya hukumu. Wao ndio wanahujumiwa na wahusika wawi. Kwa mfano katika hadithi hii ya fisi na kindi. Kindi anachukua nafasi ya muhusika mwema. Analaghaiwa na fisi *"Thoroko ri ciakurire, Kabare gakathii gagatua nthoroko. Kenukite gagatungana na Mbiti. Mbiti ikathi igatua nthoroko wabaria kabare gatuire."* Kindi alikuwa mwaminifu. Alikuwa akichuma mbaazi kwake bila kutamani za mwenzake "*Mbiti nitua gwa Kabare. Kabare nako nigatua gwake, Gwatwika riu cia mbiti itigukomwa, na tintue.*" Kindi alijitokeza kama mjinga. Hang'amui kwa haraka kubadilika kwa tabia ya fisi. Hatambui mapema hujuma na ulaghai wa fisi hadi pale mbaazi zinaelekea kuisha shambani

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

> *"Riu wa ntuku kabare gakithii mbele gagitua. Mbiti ikiuma thuuba. Magitungana. mbiti ikithii, igitua. Kabare ntuku ingi kakithii kethiria kethiria nthoroko ciako iri bakubi guthira, kamiuria "mbiti, ai umbiraga utionaga muntu u umbiaga na ni weu tutunganaga nawe ma? Utanona nwari muntu agitua nthororoko ino ciakwa nuntu iri bakubi guthira?"*

Kindi alikuwa mwenye busara. Fisi alipokana kuwa hajawahi kumwona aliyekuwa akichuma mbaazi za kindi, kindi hakuzozana naye. Alitumia mbinu rahisi na faafu ya kukabili mzozo baina yake na fisi. Alipendekeza tambiko la kuruka mto ili kutambua mwizi bila maonevu.

> *Amwira, "riu, nitutue kiatho na auke. Withiranie mbiti cionthe nan mbithiranie tubare tuunthe. Tuthi muburoni witagwa Ginci kiiru. Tuthii tutube. Uria ukagwa ku, niwe ukamenyeka niwe wiaga nhtoroko cia uria wingi."*

Kindi alikuwa mpole. Baada ya kundua kuwa fisi alikuwa akichuma mbaazi kwake hazua urugu wala fitina. Alimhoji fisi kwa upole

> *"…kabare gakithii kathiite gutua ri, gakiona Mbiti itatua kwayo, itwire gwako. Riu kabare gakithii gakiuria Mbiti," Mbiti' nuntu ni gweu urigirie ri, nuwonire uria untwirire nthoroko?"*

Hatima ya muhusika mwema ni ushindi. Kindi aliruka mto Ginci Kiiru mara tatu mbila kutumbukia. Wema wake unamwepushia adhabu na kuangamizwa na nguvu za tambiko. Muhusika mwema anaipamba hadithi kwa kuonyesha kuwa haki inaweza kupatikana bila hiana katika jamii. Anaonyesha kuwa mbinu za matambiko jadi zinaendeleza usawa na kupatikana kwa ridhaa kamili baada ya kuhujumiwa. Fisi ananaswa huku kindi akapata uwezo wa kuepushiwa adhabu.

## Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya *Ngongoana* na *Gacinci*

Wahusika katika hadithi hii walikuwa Pamoja na Ngongoana, Gacinci, kaka yao, zimwi na wacheza ngoma. Wahusika hao waligawika katika mikabala miwili. Wawi na wema.

### *Wahusika Wawi*

Wahusika wote wanatanguliza hadithi hasa kwa habari njema. Wahusika wawawi wanajitokeza katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Wahusika hao ni wale wanaosambaratisha mshikamano wa jamii.  Mwanzoni Ngongoana na Gacinci wanaishi kwa ushirikiano mkubwa ingawa ni mayatima "*Kwari na Ngongoana na Gacinci. Muntu na muru wa ng'ina."* Wanakaa pamoja kule nyumbani na kuepuka kushiriki ngoma za densi ili zimwi lisiingie nyumbani na kuwaangaisha. Wanaheshimiana. Gacinci alikuwa akitii tahadhari ya Ngongoana dhidi ya kwenda densi za usiku

> *"Riu nyimbo cia tene nuntu niciainagwa, Gacinci akera Ngongoana, "kanthii rwimbo." Ngongoana akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkariwa ni marimarimu," nuntu kwari na marimarimu. Akegua akerega kuthii.*

Gacinci na zimwi walichukua nafasi ya wahusika wawi. Gacinci alikuwa mkaidi. Aliacha kutii ushauri wa Ngongoana na kwenda kushiriki densi za usiku "*Ntuku i ingi rwainwa bakubi muno. Amwira, "Ari nee, gankegue baba ii ngakuthikagiriria ii nkegucaga irimarimu rikigita atia? rigiigica." …Athii. Akinya rwimboni"*. Gacinci alikuwa mwenye tamaa. Alitamani sana kwenda kusikiliza densi za usiku "*Amwira, "Ari nee, gankegue baba ii…."*. Alikuwa msaliti. Alidhamini sana kujiburudisha kuliko kukaa na dadake na kumlinda dhidi ya zimwi "*Athii. Akinya rwimboni. Irimarimo nario riari wa baba ruriini rikinathungira.*"

Zimwi linapochukua usukani na kuendelea na uovu, Gacinci anajigundua na kuchukua hatua ya kurudia

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

wema. Aliposikia sauti ya dadake akiteswa na zimwi alikumbuka wajibu wake wa kushirikiana na dadake. Alichukua hatua na kuanzisha harakati za ukombozi.

> *Gacinci akinegua mwang'ina akina. Akinela antu, "Takirani mbigueni." Egua …Akimera, "riu ncuni ii, mumbile nuntu riu ni irimarimu rikuthinia mwana wetu*

Zimwi badala ya kumwadhibu Gacinci kwa uovu wake, linakuwa katili na kumhangaisha Ngongoana. Linaingia chumbani kwa ulafi na kutaka maziwa yote.

> *Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua, riathiria…Riamwira, "ngundia ingi". Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria. Riu rikinamwira atiri, "Ngongoana, ngundia ingi." Arira, niriathira."*

Zimwi lina tamaa iliyozidi. Linapokamilisha kunywa maziwa linapania kumla Ngongoana. Linamtaka alibebe ili likamle "*Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria*". Zimwi lilikuwa sumbufu. Lilimsumbua Ngongoana lilipoingia chumbani na kumtaka alibebe kwa kamba kama kuni mgongoni ingawa lilikuwa na uzito uliomzidi Ngongoana. Alilibeba huku akilia "*Ngongoanga aruma mukanda oba irimarimu na atikuribota. Arikua akigucaga atikuribota.*

> Sifa mbaya za zimwi zinachochea hadhira kulichukia na kuchukia tabia kama hizo katika jamii. Hatima ya muhusika mui ni maangamizi. Zimwi linauawa kwa kuchomwa mishale na mkuki. "*Irimarimu riauma. Riambilia kurathwa na migwi, kumutangwa na matumo, riakua.*

***Wahusika Wema***

Wahusika wema ni wale wanaodumisha umbo la uzuri wa mienendo katika hadithi. Katika hadithi ya Ngongoana na Gacinci, muhusika Ngongoana anashikilia mienendo inayodumisha mshikamano wa jamii. Ngongoana ni mshauri mwema. Kila mara anamshauri dadake kukaa nyumbani na kukoma kwenda ngoma za usiku ili kusitiza zimwi kuingia nyumbani. Kwa mfano,

> *Gacinci akera Ngongoana, "kanthii rwimbo." Ngongoano akamukania akamwira, "tiga kuthii, nkariwa ni marimarimu," nuntu kwari na marimarimu. Akegua akerega kuthii.*

Ngongoana ni mpole na mtiifu. Zimwi linapoingia chumbani likamwita na kudai kupewa maziwa, allitika kwa upole na kulipa maziwa yote mbila ubishi. Zimwi lilipomtaka achukue kamba alibebe, alifanya hivyo bila ubisha ingawa hakuwa na nguvu ya kulibeba. Kwa mfano,

> *Irimarimo nario riari wa baba ruriini rikinathungira. Riamwita, "Ngongoana," arira, "wuu," "Ngundia iia." Arinekera iria na nthegu riainainia rianyua; riathiria.*
>
> *Riamwira, "ngundia ingi". Rianenkerwa ringi rianyua; riathiria. Riu rikinamwira atiri, "Ngongoana, ngundia ingi." Amwira, " niriathira."Amwira , "Ngua. Ngua ta ngu, nwa niu ngakuria. Ngongoanga aruma mukanda oba irimarimu na atikuribota. Arikua akigucaga atikulibota.*

Ngongoana alikuwa mwenye hekima. Alifahamu na kutumia mbinu ya kumtaarifu dadake bila kuhatarisha maisha. Alitumia kiitikio cha wimbo kuwasiliana na dadake na kuomba msaada wa ukombozi. Dadake aliposikia kiitikio cha wimbo, alitambua kuwa Ngongoana alikuwa hatarinikisha kuwaombo wacheza ngoma kumsaidia kumwokoa. Kwa mfano,

> *Ngongoana akiriraga muno. Akiinaga:*
>
> *(Gacinci ii Gacinci mwile ndagukanilie wathi*
>
> *Wa utuku Gacinci mwile) x3*
>
> *Akamwila, "Ngongoana ii ndwaa njia ya mumbu, ndugandwae njia ya mugumo."*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

*Rikaina: Gacinci ii Gacinci mwile*

*Ndagukanirie wathii wa utuku*

*Gacinci mwile*

*Gacinci akinegua mwang'ina akina.*

Hatima ya muhusika mwema ni ushindi. Ngongoana alikombolewa na kakake pamoja na wacheza ngoma waliokuwa pamoja na Gacinci. Zimwi linapouawa, wanaamana yeye na dadake kurudi nyumbani kwa amani. Ngongoana alifanikiwa kurejesha umoja wao na dadake kwa kurudi nyumbani pamoja. Kwa mfano,

*Riakua nirio Gacinci menukile na mwang'ina.*

**Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Wasichana Wanne wa Ukambani**

Wahusika katika hadithi hii walikuwa wasichana watatu, Mweru, Nyaga, Babu na wazazi wa Nyaga na Mweru. Wasichana watatu wanachukua nafasi ya wahusika wawi huku Mweru akitawala nafasi ya wahusika wema.

***Wahusika Wawi***

Wahusika wawi wanajitokeza katika sehemu ya hadithi ya mabadiliko ya mienendo. Wahusika hao walikuwa kiini cha kuvurugika kwa wema wa jamii. Wahusika wawi katika hadithi hii walikuwa wasichana watatu. Hadithi ilipotangulizwa wahusika wote wanaanza kwa kushirikiana na kuwa na mshikamano. Wasichana wote wanne wanakubali kwa pamoja kushiriki mradi wa urembeshwaji. Wanakubali kwa pamoja wakatiwe mwanya.

*"Airitu mana ma Ikamba meerwa ni magacawe njarumi. Mathii gucawa magego. Macawa, maca merana atiiri "Nituthii muburoni ii…."*

*Wasichana wane kutoka Ukambani waliambiwa wangechongwa meno kuyatia mwanya wa Urembo. Wakaenda kuchongwa Meno. Baada ya shughuli hiyo kukamilika, waliambiana "Twendeni mtoni…*

Wasichana watatu wenzake Mweru wanajitokeza kuwa wahusika wawi baada ya kushindwa na Mweru. Ni wasichana wenye kinyongo. Walimwonea Mweru wivu baada ya kuwa na mwanya mzuri kisha kupanga njama ya kumuua badala ya kumpongeza.

*Mathii kuri antu monete irima iraca muno muntu akibingirwa ku akaurira ku. Mathii ri, mathiuba mbele ya Mweru makinacirira mari mathatu merana "nituthii turugure ibari (ibiga ri rikunikite) twikire mweru ku, na twekira mweru ku agakuira kuu.*

*Wakaambiana, "Twendeni tufunue shimo kwa kuondoa lile jiwe tumrushe Mweru ndani. Na tukimtia mle, atafia humo.*

Kutokana na kinyongo watatu hao wanakuwa wenye chuki. Wanamchukia Mwenru na kuanza kumtenga katika ushiraka wao. Walipiga hatua mbele kwa haraka ili kumwacha Mweru kwa nia ya kumpangia njama ya kumwangamiza.

*Mathii ri, mathiuba mbele ya Mweru makinacirira mari mathatu merana "nituthii turugure ibari (ibiga ri rikunikite) twikire mweru ku…*

*Walipoenda, wakaharakisha hatua mbele ya Mweru kisha wakakubaliana wakiwa watatu, "twendeni tuinue jiwe tumtumbukize Mweru mle.."*

Watatu hao waliacha kuwa waaminifu na kuwa wasaliti. Wanakubaliana kuuingia shimoni na kwa zamu kisha kutoana kwa kwamba ila Mweru alipofikiwa na kuingia shimoni walikosa kuvuta kamba na kumwacha mle. Badala yake wanamfunikia mle ndani kwa jiwe.

*Makinerana, "nitumuthairirie ii, turume mukanda, twaruma mukanda, muntu athungira akaburutwa ni antu mathatu akauma. Indi*

This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

East African Journal of Swahili Studies, Volume 6, Issue 1, 2023
Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

> *muntu wa cietu ambe athungire ari wa mbele, kenda mweru akarigia akiugaga akarutwa turege kumuruta."*

> *Wakasemezana, "Tumdanganye. Tuchukue Kamba. Mtu mmoja akiingia, anavutwa na wale watatu anatoka. Mmoja wetu atangulie ili Mweru aingie akiwa wa mwisho. Halafu tukatae kumwondoa mle.*

Wasichana wale watatu walibadillika na kuwa watu waongo. Walikubaliana kwa pamoja kundanganya kuwa Mweru aliliwa na fisi ambao walikuwa wengi katika eneo hilo kipindi hicho.

> *Na twinukange na karugi muno, twathii tuge atiri, nuntu kwina mbiti, twaurua tuge nimbuga karirwe ni mbiti nuntu niwe enukire mbele yetu".*

Kisha turejee nyumbani haraka sana. Tukiulizwa kuhusu habari yake, tuseme alitangulia na huenda alililiwa na fisi."

Hatima ya mhusika muwi ni maangamizi huku ukweli ukibainika na wenye haki kuipata. Wasichana watatu wawi wanaangamia kwa kubadilika kuwa vipepeo baada ya Mweru kuandaa tambiko la kinywaji kilichotiwa ghudi ya kunasia ndege. Ukweli ulibainika baada ya uvumbuzi wa Nyaga ndugu yake Mweru na Mweru kuokolewa na wanajamii.

> *Mweru riu karimurakaru. Gakwenda kumaita. Atigwa, ariba urembo wa muremangige. Ariba urembo uunthe. Amenya iria riria akamanenkeera rikegua rina urembo.*

> *Maca Kiatho mamukirwa ni Mweru ringi. Makundua Iria. Iria riria magakundua ti yega. Mweru akunda ri yeega. Manyua ingi makiugaga makunyua monthe. Riu akinamera "tuthiini nimukinyieni." Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe.*

***Wahusika Wema***

Wahusika wema ni wale wanaodumisha wema wa kijamii pamoja na kuendeleza mshikamano wa mfumo wa jamii. Katika hadithi ya Wasichana wanne wa Ukambani, wahusika Mweru, Nyaga, babu na wanajamii walikuwa kiwakilishi cha wahusika wema. Mweru alikuwa mpole na mshirika mwema. Baada ya kuwashinda wenzake na Mwanya wake kubainika kuwa mzuri hakuwatenga wala kuwadharau wenzake watatu. Aliendelea kushirikiana nao kama walivyozoea.

> *Mweru we atacawa riingi nuntu we niamacindite. Maca riu merana "Riu ni gutua ringi". Mambiriria kugera munyiri ringi. Magera magera magera matikubetukia nwaka makugwithia runcini mari mathatu ringi. Mweru atua aringia ringi.*

Mweru ni mwepesi wa kuwaamini wenzake. Yeye na wenzake walipokubaliana kuingia shimoni kisha kila mmoja kutolewa na wengine kwa kuvuta kamba hakuwa na ubishi kuwa wa mwisho kuingia. Alipowaamini na kuingia wakakosa kumtoa ingawa alifanya hivyo kwa kuwaamini.

> *Mabanga ugu. Mathungira ria mbele makirutanaga makirutanaga makirutanaga. Marutana monthe kinya ona mweru maruta. Macokera ria kairi. Mathii mathatu akirutagwa. Mweru arigia. Arigia ri, akiinamia mukanda arutwa ri, akunikirwa na ibari (ibiga)*

Mweru pia, alikuwa karimu. Wasichana wenzake walitambua kuwa aliokolewa waliamua kwenda kumsalimia, hata hivyo Mweru aliwakaribisha na kuwakirimia kinywaji bila kujali walivyomtenda uhayawani.

> *Mathii Kumukethia ntuku ya mbele, Mweru amamukiira wega muno na nkinya amakundia iria manunyanira weega muno.*

Mweru ni mpambanaji na mstahimilivu. Alipambana na hali ngumu mle shimoni pamoja na kustahimulili uozo kwenye mguu bila kukata tamaa. Alipoitambua sauti ya Nyaga aling'ang'ana hadi

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

kuhakikisha Nyaga amemtambua na kumsaidia. Aliimba kwa sauti ili Nyaga asikie na kumwokoa. Hatimaye anafaulu na kuokolewa na wanajamii.

> *Nawe kaana karia gekaririte ibaari riri, gatikumenya kana ni ibiga rikunikanie. Gekarite o baria Mweru ari. Mweru egua akinaina: ...*
>
> *Nyaga abanga "ari kambire mburi iria bu ringi"*
>
> *Amiira "Mburi iria uroura ukaura ta Mweru uria wetu waurire."*
>
> *Akinegua:*
>
> *Nkanga ii nkanga cia Maindi*
>
> *Gacirici nyaga wetu nkanga cia maindi*
>
> *Wana riu nwa tutwire*
>
> *Nkanga cia maindi*
>
> *NItwarire nguo cia mwili*
>
> *Nkanga cia Maindi*
>
> *Tukinora mugwanja umwe*
>
> *Nkanga cia Maindi.*

Hatima ya wahusika wema ni kupata ushindi na ukombozi kama haki. Mweru alikombolewa na wanajamii na kurudia hali yake ya kawaida baada ya kutunzwa na kupona uozo. Ukweli unabainika kuwa hakufa bali alitupwa shimoni. Wenzake wanabadilika kuwa vipepeo huku Mweru akibaki kufurahia mwanya wake mzuri.

> *…makinegua Mweru ri, niarabwire. Niaronire wa kumuruta kuu irimani. Makinandika kamakamukethie. Mathii Kumukethia ntuku ya mbele, Mweru amamukiira wega muno na nkinya amakundia iria manunyanira weega muno. Riu ri, amakinyia menuka. Akinamatwira kiatho na auke. "Muce na nkegua nimukuirite ii, wana iria ni mukethira riri bo." Amera "nibe tugaca gugukethia Mweru."*
>
> *Mweru riu karimurakaru. Gakwenda kumaita. Atigwa, ariba urembo wa muremangige. Ariba urembo uunthe. Amenya iria riria akamanenkeera rikegua rina urembo.*
>
> *Maca Kiatho mamukirwa ni Mweru ringi. Makundua Iria. Iria riria magakundua ti yega. Mweru akunda ri yeega. Manyua ingi makiugaga makunyua monthe. Riu akinamera "tuthiini nimukinyieni." Amakinyia magikinya njirani mambiriria gutwika iburiti monthe. Mweru atigwa na mwanya wawe.*

**Sifa za Wahusika wa Kisimulizi Katika Hadithi ya Fisi na Ndovu**

Wahusika katika hadithi hii walikuwa fisi na ndovu. Wahusika hao waligawika katika mikabala miwili. Wawi na wema.

***Wahusika Wawi***

Wahusika wote wanatanguliza hadithi hasa kwa habari njema. Wahusika wawi wanajitokeza katika sehemu ya pili ya matukio ya hadithi. Wahusika hao ni wale wanaosambaratisha mshikamano wa jamii. Mwanzoni fisi na ndovu wanaishi kwa ushirikiano mkubwa.

> *Njogu na mbiti ni ciatumite urata. Cierana, riu niilalage irimani rimwe. Ciatua kuraraga irimani rimwe. Njogu yari na twana twayo na mbiti yari na twana twayo.*
>
> *Ndovu na fisi walikuwa marafiki wakubwa, wakakubaliana wawe wanalala na kuishi kwenye shimo moja. kila mmoja alikuwa na wanawe lakini wote waliishi kwa Amani.*

Hatima ya muhusika mui ni maangamizi. katika hadithi tunapata kuwa mhusika fisi na wanawe ambao ni wawi wanaangamizwa kwa kupigwa mateke na kukanyagwa na ndovu.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

*Mbiti yakira. Mbiti yambatwa. Yakinyithanua ni njogu yakua. Twana twambatwa. Twakinyithanua twakua.*

*Fisi akanyamaza. Akashikwa na tembo. Akakanyangwa akafa. Wanawe wakashikwa. Wakakanyangwa wakafa*

***Wahusika Wema***

Wahusika wema ni wale wanaodumisha umbo la uzuri wa mienendo katika hadithi. Katika hadithi ya fisi na ndovu tunapata kuwa wana wa tembo wana sifa za mhusika mwema kwani tunapata ya kuwa hawakuwadhulumu wana wa fisi hata kama walishambulia ndugu zao.pia tunapata kuona mwana mmoja wa tembo anaamua kwenda kumuarifu mama yake waliyokuwa wanapitia mikononi mwa rafikiye fisi na vikembe wake. Alifunga safari hadi alikokuwa malishoni.

*Mwandovu aliyekuwa na chongo akatanabahi kuwa wamebaki wawili tu. Akasema, "tutaenda malishoni kula na wana wa fisi. Lakini, kwa kuwa sijui iwapo ni mie au ndugu yangu ataliwa na fisi nitatoroka. Sitasubiri tuliwe sote. Nitaenda kumsaka mama aishiko. Nitakua nikila mbali na fisi pale kichakani. Sitawafuata wakirejea pangoni. watamla ndugu yangu ila mimi watanifuata wanikose. "akaamua.*

*Wakaenda malishoni kama ilivyokuwa mazoea. Yule chongo akasafiri mchana kutwa. Ndugu yake akarejea pangoni na kuliwa na wana wa fisi. Fisi na wanawe walidhani kwamba yule chongo angerudi. Lakini alikua ameapa, "sasa ni kwenda bila kuangallia nyuma."*

*Akasafiri hadi akakutana na fisi. Akaimba:*

*fisi mnaokula huku, mnaokula huku,*

*mumemwona tembo aitwaye cianyaga?*

*Alituacha katika nyumba ya fisi.*

*Mwanafisi akasema, m…m…m…m…*

*Akaulizwa nini kinachokuliza?*

*Akasema nalilia mwana yembo.*

*Ng'ata ila using'ate kwa nguvu.*

Hatima ya muhusika mwema ni ushindi. Fisi anaangamizwa nakuleta ushindi katika familia ya ndovu na wanawe wawili kwani waliweza kuokoa maisha yao.

**HITIMISHO**

Lengo kuu la Makala haya lilikuwa kujadili sifa za wahusika wa kisimulizi zilivyoendelezwa kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Matokeo yalithibitisha kuwa wahusika hugawika mara mbili kiujumi katika ngano simulizi za Wachuka. Wahusika wema na wawi ambao sifa zao hutumika kuendeleza ujumi katika ngano simulizi za Wachuka.

**MAREJELEO**

Bakhtin, M. (1981). The Dialogic Imagination (C. Emerson & M. Holquist, Trans.)

Foley, J. M. (1995). *The Singer of Tales in Performance*. Bloomington and Indianapolis

Hymes, D.H. (1970). Linguistic method in ethnography: Its development in the United States. In P. Garvin (Ed.), *Method and theory in linguistics*. The Hague: Mouton.

Harmon W., & Holman, H. (2000). *A Handbook of Literature ( 8th Edition)* . Upper Saddle River: Prentice Hall.

Hegel, G. (1997). *Introduction to Aesthetics.* London: Oxford University Press.

Madumulla, J. (2011). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historian a Misingi ya Uchambuzi.* Dar es Salaam: Mture Educational Publishers.

Mathooko, P.M (2006). Fasihi Simulizi: Chombo Hifadhi cha Lugha za Kiafrika. Katika K.

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.

Article DOI: https://doi.org/10.37284/jammk.6.1.1467

Njogu, Momanyi C & Mathooko P.M (wah), *Fasihi Simulizi ya Kiswahili*. Nairobi: Twaweza Communications

Mutiso, K. (2005). Utenzi wa Hamziyyah (The Hamziyyah Epic. A Detailed Analysis of a Swahili Islamic Epic). *Institute of Kiswahili Research, University of Dar-es-Salaam, Dar-es-Salaam, 2005; 360+ 15 pp*.

Njogu, K., & Chimerah, R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation .

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi, Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers.

Wamitila, K. (2003). *Kamusi ya Fasihi : Istilahi na Nadharia* . Nairobi: Focus Publications.

Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi Simulizi na Andishi.* Nairobi: Focus Books.

Simala, I. (2006). Fasihi Simulizi Katika Enzi za Utandawazi katika. In Njogu et al, *Fasihi Simulizi ya Kiswahili* (pp. 11-18). Nairobi: Nairobi Twaweza Communications

 This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.